# Learning by Ear – Religious Dialogue: "A Bridge over Gori"

# Episode 07: "Kanisa moja:Mungu Mmoja"

**Author: Romie Singh**

**Editors: Katrin Ogunsade, Naïma Guira**

**Proof reading: Natalie Glanville-Wallis**

**Expert on African religions: Jean-Félix Belinga Belinga**

**KISUAHELI ERIC PONDA/THELMA MWADZAYA**

**List of characters for episode 7:**

- Narrator /Philip, male (17)
- Harry, male (17)
- Marian Okru, female (16)
- Preacher, Reverend Immanuel, male (40)
- Layla, female (16)
- Hassan, male (12)
- Ishmail Omer, Layla's father, male (43)
- Sister Rebecca, female (28)
- + Church congregation
- + Students in library

1. **SIG TUNE UP**

2. **INTRO**:

**Hujambo na karibu kwa sehemu ya saba ya mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga maisha yako, tukiwa bado katika ule mchezo wa Radio wa *Daraja la Gori*,. Hadithi hii ya kusisimua inaelezea jinsi Siasa na Dini zinavyoweza kueneza chuki na uhasama baina ya Jamii mbili na Familia mbili za mji wa Gori. Ungana na mabingwa wetu wachanga wanaojaribu kuusuluhisha mzozo unaoaminika kuwa umekita mizizi.Katika kipindi cha leo ambacho mada ni“Kanisa moja:Mungu Mmoja”, utasikia ikiwa Hassan,mdogo wake Layla wa kiume , atafanikiwa kuubadili mtazamo wake wa Muuguzi wa kiyahudi,Dada Rebecca, na kama Harry atazama katika wimbi kubwa linalomuandama shuleni, kinyume na alivyotarajia... Philip ni rafiki mkubwa wa Harry na msimulizi wa hadithi hii… Endelea kuwa nasi hadi mwisho!**

## Scene 1. Under Gori Bridge

**Philip, Harry, Layla**

**3. PHILIP/NARRATOR: Hapakuwa na shaka kuwa Hassan, mdogo wake Layla anatuhumiwa kuhusika na uhalifu wa kuliteketeza kanisa la Katoliki la Dayosisi ya Kasisi Barnabus mjini Gori.Matumaini ya Baraza la Waislamu ya kupewa idhini ya kujenga msikiti kwenye ardhi hiyo yalizidi kufifia.Kisa hiki kinampa nafasi nzuri kasisi Barnabus, Babake mdogo Harry, ya kuungwa mkono na baraza la maendeleo mjini Gori na kupewa kibali cha kuendelea na mipango ya kujenga kanisa katika ardhi hiyo. Hayo alimdokezea Babangu Daniel Layton-Browne, mhariri mkuu wa Gazeti la Tribune. Uhusiano baina ya Waislamu na Wakristo katika mji wa Gori unazidi kuharibika.Kila alasiri baada ya kutoka shuleni, Harry na Layla – ambao ni vijana wa Kikristo na Kiislamu hukutana chini ya daraja la Mto Gori.**Kila **walipokutana waliujadili umuhimu wa Ubuntu,na wakagundua kuwa kila mmoja anamjali mwenzake…jambo lililonivunja moyo kabisa.**

4. <u>SFX: River flowing, birds, cars passing by in a distance</u>

5. **HARRY:** Mpenzi Layla , "Niko nilivyo kwa sababu yako wewe".

6. **LAYLA:** Nikumbatie, Harry...!

7. **PHILIP/NARRATOR:** Jinsi maji ya Mto Gori yalivyotiririka taratibu,fikra ilinijia… iwapo ninamtaka Layla awe wangu sina budi ila kumwekea mtego Harry.Marian ambaye anaikaimu nafasi ya Layla katika kundi la mjadala ndiye atakayekuwa chambo changu!!…kwasababu anampenda Harry!

**<u>Scene 2. First outside and then inside the Charismatic church</u>**

**Marian, Harry, Preacher, congregation**

8. <u>SFX: Loud singing of Christian songs from inside the church</u>

9. **MARIAN:** Hah, Harry! Nilikuwa na matumaini makubwa kwamba utauridhia mualiko wangu ujionee jinsi sisi wafuasi wa kanisa huru la Imani moja tunavyoabudu.Tuingie ndani,Mchungaji Henry Immanuel ameanza ibada.

**10. HARRY:** **Oooh , Marian, lile ni gari lake,..? ni kubwa sana?**

**11. MARIAN:** **Ndio, ni gari lake, zawadi kutoka kwa wafuasi wake!. Pia mimi nilichangia. Naamini mchango wangu ulitumiwa kuunua mto wa hariri ulio kwenye kiti cha nyuma.**

**12. HARRY:** **Lakini waumini hawa wanaonekana watu maskini sana. Waliwezaje kuchanga namna hiyo?**

**13. MARIAN:** **Wanaweza kumchangia hata kama ndiyo sarafu yao mwisho. Mhubiri Immanuel ni Mtume na anaweza kutuokoa sisi sote.Ingia ndani uokolewe**.

**14. <u>SFX: Door opening, entering church. Door closes. Clapping/singing/ wailing/ ululating.</u>**

**15. PREACHER's VOICE:** **Njooni hapa mbele muokolewe.Mungu yu nanyi..!.Tuna azma ya kukusanya zaidi ya dola elfu tano… ndio …Dola elfu tano mahsusi kwa kazi ya Mungu..!**.W**anaotoa kwa moyo wote,Mungu atawapa uzima wa milele.**

**16. MARIAN:** ***(whispers)*** **Hebu- subiri nikuvalishe hii kwenye shingo yako Harry! Hii ni kumbukumbu ya Mungu mmoja wa kweli.**

**17. HARRY:** ***(whispers)*** **Ni nini hiki?**

**18. MARIAN:** **Ni mkufu tu wa dhahabu ulio na msalaba..**

**19. HARRY:** **Lakini haturuhusiwi kuvaa vitu vinavyoashiria dini shuleni.**

**20. MARIAN:** **Hatuko shuleni hapa Harry,uko ndani ya nyumba ya Mungu.**

**21. HARRY:** **Hebu sikiliza hapa.. Sidhani Mhubiri Henry anahaki ya kujiita Mtume,au hata kupokea pesa za watu maskini kama hawa.Amewafanyia mazingaombwe wote! Hebu watazame.!**

**22. <u>SFX: ululating and ecstatic screaming comes up</u>**

**23. MARIAN:** **Hapana wamejawa na Roho Mtakatifu.**

**24. HARRY:** **Lakini Roho Mtakatifu hamtozi mtu ada.Wanadanganywa ili wazitoe pesa zao na hilo si sahihi. Mtumishi wa Mungu anapaswa kuwasaidia watu maskini na wala sio kuvichukua walivyonavyo.**

**25. MARIAN:** **Kanisa letu ni la Imani Moja. Tunatoa kwa hiari!**

**26. HARRY:** **Naendoka sasa.Tutaonana shuleni siku ya Jumatatu.**

**27. <u>SFX: steps leaving on stone floor, church door opens and closes</u>**

**28. <u>BRIDGING MUSIC</u>**

**29. PHILIP/NARRATOR:** **Wakati huo huo Layla alitaka kuzungumza na Babake kuhusu Hassan. Bado anakataa kula na kunywa dawa Hospitalini kwasababu hataki huduma za mhudumu Myahudi, Dada Rebecca.Hata hivyo Rebbecca ameyapuuza hayo yote na hajakata tamaa. Layla amejawa na wasi wasi.Kwa bahati nzuri Mzee Omer amefika nyumbani mapema siku hiyo na akapika chakula kizuri wale na binti yake**

**Layla.Hakuwa na mambo aliyokuwa yakimsumbua kwahiyo alikuwa tayari kuzungumza na pia- kusikiliza.**

**<u>Scene 3. At the Omer's</u>**

**Layla, Mr. Omer**

**30. <u>SFX: Eating dinner, soft Islamic music in the background, dishes clattering, pouring some juice into glasses</u>**

**31. LAYLA:** **Baba .Ahsante sana kwa kinywaji hiki cha maembe na chakula kitamu! Kinanukia vizuri!Lakini *(voice changing to a sad tone)* sasa tuzungumze kuhusu mdogo wangu. Hassan anakataa kuhudumiwa na Dada Rebecca kwa kuwa ni Myahudi. Anasema kuwa Rebbecca ni miongoni mwa watu waliomo kwenye kitabu.**

**32. MR OMER**: **(talking with full mouth) Myahudi? Mhudumu Rebecca ni Muyahudi?. Kwahivyo? Huyo ndiye aliyeyaokoa maisha yake! Ole wangu! Lakini Hassan ameyapata wapi mawazo haya mabaya? Familia yangu kamwe haiwatazami marafiki zetu wasiokuwa waislamu kama makafiri'.**

**33. LAYLA:** **Hassan ana umri wa miaka 12 tu Baba. Anaweza kubadilika akielekezwa vizuri.Lazima tuwe na muda mwingi naye. Tangu mama afariki Hassan amekuwa mpweke sana.!. Nadhani wale vijana wengine wa Madrassa wanautumia mwanya huo kumvuruga.**

**34. MR OMER:** Kipi bora cha kufanya **Layla?**

**35. LAYLA:** **Tunahitaji kutumia muda zaidi kukaa na yeye ili tufuatilie kwa karibu mambo anayofanya,vitabu anavyovisoma. Mtoto ambaye anajihisi familia yake inamjali kamwe hawezi kuhusika na vitendo vya kuteketeza makanisa. Dada Rebecca ni mhudumu mzuri na nina hakika anataka kumsaidia Hassan!.**

**36. BRIDGING MUSIC**

**Scene 4. In hospital**

**Sister Rebecca, Hassan**

37. <u>**SFX: Hospital ambience, sister Rebecca opening Velcro-strip of blood pressure meter**</u>

38. **SISTER REBECCA: Hassan, nyosha mkono wako nataka kupima msukumo wako wa damu mwilini!. Tafadhali si mimi ni rafiki yako?.**

39. <u>**SFX: some rustling and pumping of pressure sleeve**</u>

40. **HASSAN: Sitaki urafiki wako.**

41. **SISTER REBECCA: Hassan. Mimi ni muuguzi. Nitakusaidia kupata nafuu.**

42. <u>**SFX: Air from blood pressure meter passing of slowly**</u>

43. **SISTER REBECCA 80 juu ya alama 120. AHhhh! Kweli kiwango cha msukumo wako kiko sawa sasa.**

44. <u>**SFX: Opening Velcro-strip of blood pressure meter**</u>

45. **SISTER REBECCA: Sikiliza Hassan . Sisi wanadamu tuko hapa duniani kutenda yaliyo mema. Hata dini inatueleza hivyo.! Dini yangu inanifundisha hayo. Na, naweza kutenda mema kwa kukusaidia upoe.**

**46. HASSAN:** **Niliambiwa wayahudi ni makafiri.**

**47. SISTER REBECCA:** **Hassan – Sisi sote ni watoto wa Mungu, na tunapaswa kujiamulia ni dini gani tunayotaka kuifuata. Lakini kama wewe utazingatia tofauti za watu binafsi na wala sio Ubinadamu, daima utakuwa huna raha maishani.**

**48. HASSAN:** **Wewe ni myahudi. Hupendi waislamu hata kidogo…!**

**49. SISTER REBECCA:** **Si kweli, Dini yangu inanifundisha kwamba Muislamu na Myahudi wanamuabudu Mungu mmoja na sisi sote ni kizazi cha Abraham. Mji wa Jerusalem ni mji mtakatifu kwa waislamu …… na pia kwa Wayahudi . Sisi sote ni tuna chimbuko moja. Watoto wa Abraham, Hassan… unasikia.**

**50. HASSAN:** **Mimi nataka nife tu niwe pamoja na Marehemu mamangu.!.**

**51. SISTER REBECCA: Hassan,naamini Mungu ndie anayetupa uhai,… Maisha yako yana thamani kubwa, usiyadharau.Qu'ran tukufu ina aya inayosema …Na musijiuwe. Allah ni mwenye huruma nyingi."**

**52. HASSAN: *(crying)*Sistahili huruma!**

**53. SISTER REBECCA: Hilo si kweli ,unazihitaji huruma zake. Lazima kwanza ujisamehe.**

**54. Singing softly a sweet African song (local lullaby)**

**55. HASSAN: Mikono yangu inaniuma, tafadhali nisaidie! Tafadhali?.**

**56. SISTER REBECCA: Sawa!**

**57. SFX: opens bottle**

**58. SISTER REBECCA: Wache nikupake malham!**

**59. HASSAN:** *(in pain)* **Oh! Ouch!** ***(Sigh)*** **Hah!…maumivu yametulia.**

**60. SISTER REBECCA:** Barabara kabisa! **Sasa jinyooshe hapa ili ulale vizuri ..!**

**61. HASSAN:** **Ahsante…...**

**62. SFX: Footsteps leaving, door opens, closes**

**63. BRIDGING MUSIC**

**64. PHILIP/NARRATOR:** **Wakati huo huo, Chuoni… mtego niliomuwekea Harry ulichukua mwelekeo mpya baada ya Marian kunifuata kwenye maktaba.…**

**Scene 5. In the school library**

**Marian, Philip**

**65. SFX: students murmuring in the background, books being placed on tables, turning book pages, paper rustling**

**66. MARIAN:** *(whispers)* **Philip. Harry amevaa mkufu wenye msalaba shingoni.**

**67. PHILIP:** **Uhhhh? Imekuaje , Marian?**

**68. MARIAN:** **Nilimpa jana kanisani…! Nadhani amesahau kwamba bado anao shingoni. Layla akiuona atahamaki kweli!Na hapo nitapata nafasi ya kuwa na Harry na wewe uweze kumrudia Layla kama ulivyotaka!**

**69. PHILIP:** **Sawa.Ondoka sasa Marian. Ninaandaa mpango ila sitaki atuone tukiwa pamoja.Ondoka sasa**

**70. <u>SFX: Marian leaving, steps leaving fast</u>**

**71. <u>BRIDGING MUSIC</u>**

**72. PHILIP/NARRATOR:** **Marian alisema kweli, huu ulikuwa wakati muafaka wa kuuvunja uhusiano wa Harry na Layla.Akili yote ya Harry ilikuwa kwenye hesabu alizokuwa akidurusu hata hakugutuka nilipomtaka anionyeshe mkufu aliokuwa nao shingoni.Aliuvua bila hata ya kupesa jicho! Niliuchukua na kuuhifadhi mfukoni mwangu bila ya fahamu zake!**

**73. <u>SIG TUNE UP</u>**

**74. OUTRO:**

**Na hadi hapo ndipo tumefika mwisho wa makala hii ya saba ya mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo-Jenga Maisha Yako ya mchezo wa "Daraja la Gori‖. Ungana nasi kwa sehemu ya nane ufahamu yatakayojiri, iwapo Harry atanasa kwenye mtego wa Philip!Kumbuka ukiwa na maoni au ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki na vyengine vinavyotayarishwa na Deutsche Welle, tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.**

**End of Episode 7**